



PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA

P.O. Box 55666
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Tel: +255 754 942 678

Email: info@pst.or.tz

20/08/2022

TAARIFA KWA WAFAMASIA NA WADAU WA SEKTA YA DAWA NCHINI

**YAHUSU KIKAO CHA WIZARA YA AFYA NA CHAMA CHA WAFAMASIA TANZANIA
KILICHOFANYIKA TAREHE 19 AGOSTI, 2022.
OFISI NDOGO ZA WIZARA
NIMR DAR ES SALAAM**

Uongozi wa Chama cha Wafamasia Tanzania (PST) ulipata fursa ya kufanya kikao na Waziri wa Afya Mh. Ummy Mwalimu. Mh. Waziri aliambatana na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mfamasia Mkuu, Msajili Baraza la Famasi, Mkurugenzi Mkuu NHIF, na maafisa wengine wa Wizara. Mheshimiwa Waziri alitumia mkuano huo kutoa mwelekeo wa serikali katika sekta ya afya nchini na kusisitiza katika maeneo makuu mawili;

- Ubora wa Huduma(Quality of Care)**
- Upatikanaji wa Huduma (Availability/Acces to Care)**

Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba pamoja na jitihada za serikali, bado zipo changamoto katika ubora wa utoaji huduma (service delivery) mfano; Huduma za kitabibu kutofanywa kwa ukamilifu wake (incomplete clinical services), Usimamizi mbovu wa bidhaa za afya (insufficient health commodities management), huduma kwa wateja isiyoridhisha (unsatisfactory customer care) na muda mrefu wa kusubiri huduma. Mheshimiwa Waziri alisisitiza kwamba ni azima ya serikali kuona kila Mtanzania anakua na Bima ya afya, ambapo kwa sasa ni 8% tu ya Watanzania ndio wako katika Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF). Mheshimiwa waziri amewataka wataalamu kuelewa mantiki ya bima ya afya kwa wote na kuwa mstari wa mbele kuielezea kwa umma.

Mheshimiwa Waziri, alieleza jinsi hali ya NHIF isivyo nzuri, na kwamba bila kuchukua hatua, NHIF inaweza kufa Mwaka 2025. Mambo ambayo yamebainika kuwa watesi wakuu wa NHIF ni pamoja na Uchache wa wachangiaji, Ongezeko la wanachama wenye magonjwa sugu, Wanachama wa hiari kujiunga pale tuu wajuapo wana magojwa sugu na udanganyifu mkubwa unaofanywa na watoa huduma walioaminiwa na NHIF.

Mheshimiwa Waziri pia ameitaka PST kujipima na kuona jukumu lake ni lipi katika kutatua changamoto hizo hapo juu. Pamoja na hayo alisema Wizara yake iko tayari kusikiliza hoja

EXECUTIVE

President
Fadhili Hezekiah.

Vice President
Mtani Njeger.

Honorary Secretary
Benson Katundu.

Deputy Secretary
Modekai William.

Treasurer
Jannette Senkondo.



PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA



P.O. Box 55666
Dar-es-Salaam, Tanzania.



Tel:
+255 754 942 678



Email
info@pst.or.tz

za wafamasia na kukaribisha uongozi kuwasilisha hoja zao. Katika kikao hicho, PST iliwasilisha hoja nane (8) kama ifuatavyo:

1: Kanuni ya Umbali wa Famasi Jamii toka Vituo vya kutolea huduma za Afya vya Umma ya mwaka 2020 (Community Pharmacy 2022 Regulation)

Maazimio

- Kanuni ipo kisheria na ina hatua zake za kuiboresha , kwa sasa ibaki hivyo huku Mheshimiwa Waziri akipata ushauri zaidi kutoka baraza la famasi na
- Famasi husika hazitahuisha vibali kwa sasa mpaka ushauri ukamilike na PST itahusishwa katika kutatua changamoto hiyo.
- Aidha Mh. Waziri alielekeza kutotolewa kwa vibali vipyta kwa maduka mapya katika maeneo ya vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali.

2: Sifa za Udhili katika vyuo vya kati.

Maazimio

- Kutaitishwa kikao cha pamoja na wadau wengine mwezi Septemba wakiwemo (APHECOT)

3: Utambuzi wa Ubobezi katika taaluma ya Famasi.

Maazimio

- Muundo umepitiwa upya na sasa unatambua ubobezi katika famasi
- Muundo huu umeshatiwa saini na Mheshimiwa Rais
- Barua za uhamisho wa wafamasia wabobezi zifuatiliwe ili waende kule wanakoweza kutumika kwa tija

4: Mapendekezo ya maboresho ya Muundo wa utumishi na ikama kwa taaluma ya Famasi

Waziri alielezwala changamoto na athari kubwa inayotokea kwa kuwa na upungufu mkubwa wa wafamasia na wataalamu wengine wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kama ilivyo sasa.

Maazimio

- Mapendekezo yamepokelewa, japo muundo umeshapita, uangaliwe utaratibu wa kuyabeba ili kitengo cha huduma za dawa wizara ya afya kiwe kurugenzi ya huduma za dawa
- Mfamasia Mkuu aanze kuutekeleza kwa kupanga watu husika kulingana na mapendekezo ya muundo uliopendekezwa na PST na maboresho yatakayofaa

EXECUTIVE

President

Fadhili Hezekiah.

Vice President

Mtani Njeger.

Honorary Secretary

Benson Katundu.

Deputy Secretary

Modekai William.

Treasurer

Jannette Senkondo.



PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA



P.O. Box 55666
Dar-es-Salaam, Tanzania.



Tel:
+255 754 942 678



Email
info@pst.or.tz

- Ikama itapitiwa upya na PST watashirikishwa ili kuona uwezekanao wa kuajiri wataalamu wa dawa mpaka ngazi ya zahanati.

5: Usimamizi wa huduma za kifamasia katika kliniki za kibingwa (Polyclinics and Specialized or Medical Clinics)

Maazimio

- Hoja imepokelewa, Mheshimiwa Waziri atapata ushauri zaidi juu ya hili

6: Uboreshaji wa huduma za kifamasia kwa kuanzisha huduma za kifamasia za kitabibu (Clinical Pharmacy Services)

Maazimio

- Muundo mpya unatambua ubobezi wa wafamasia, hivyo itachochea wafamasi kuboea
- Wizara itaongeza udhamini na kuwataka wafamasia mahospitalini kusoma clinical pharmacy

7: Athari za usitishwaji matumizi ya form 2C ya Bima ya Afya ya Taifa na mapendeleko ya Chama cha wafamasia kusaidia mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa na Wizara.

Maazimio

- Kwa hali ya NHIF ilivyo sasa, form 2C zinaendelea kusimamishwa ili kutoa nafasi ya kuboresha mifumo.
- Waziri alimuagiza Mkurugenzi wa NHIF kuajiri wafamasia wa kutosha ili kuwepo na uwiano baina ya madaktari na wafamasia waliopo katika ofisi zao na angalau kila mkoa na wilaya ili kusaidia katika ukaguzi na uhakiki

8: Usimamizi wa Weledi na Uwajibikaji katika taaluma ya Famasi, na hatimaye upatikanaji wa bidhaa za afya

Maazimio

- Kada nyingine za afya hawataruhusiwa kusoma mafunzo ya muda mfupi ya famasi na kumiliki ADDO kwa sababu ya mgongano wa maslahi
- Mafunzo ya muda mfupi hayataruhusiwa badala yake watumike medicine dispensers, assistants na pharm technicians
- Maduka yaliyopo sasa hayatafungwa, isipokua yanayokiuka taratibu.
- Baraza la famasi kuongeza kigezo cha kuhuisha kibali cha DLDM ni lazima mmiliki awe na mtoa huduma ambae ni medicine dispenser, pharm assistant au pharm Tech ili kuhakikisha wataalam wa dawa wanaiokoa jamii kutokana na tatizo la AMR.
- Baraza la Famasi lioneze waajiriwa ili waweze kufanya usimamizi ipasavyo, hata kama ni kwa mkataba.

EXECUTIVE

President

Fadhili Hezekiah.

Vice President

Mtani Njeger.

Honorary Secretary

Benson Katundu.

Deputy Secretary

Modekai William.

Treasurer

Jannette Senkondo.



PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA



P.O. Box 55666
Dar-es-Salaam, Tanzania.



Tel:
+255 754 942 678



Email
info@pst.or.tz

- Baraza la Famasi lisikasimishe majukumu ya usimamizi wa taaluma kwa halimashauri
- Baraza la Famasi watoe orodha na majina ya wafamasia na wamiliki wa famasi zote na ADDO zote kwa PST ili isaidie ufuatiliaji wa wanataaluma waliopo katika maeneo hayo ili kudhibiti kiukwaji wa maadili ya kitaaluma katika kutoa huduma

9: Uanzishwaji na ukuaji wa viwanda vya dawa umekua ukizoroteshwa na mlolongo mrefu, gharama na vigezo vingi toka mamlaka husika.

Maazimio

- Mheshimiwa Waziri atapanga kikao na TAPI na TPMA, PST wataalikwa

10: Mengineyo

Ombi la Mgeni Rasmi Scientific Conference - limepokelewa na litafanyiwa kazi

WITO KWA WAFAKASIA

1. Usimamizi wa bidhaa za afya ikiwemo dawa ni jukumu letu, hatupaswi kuwaachia wasio wanataaluma
2. Kumekua na visa vya ukiukwaji wa taratibu vinavyofanywa na baadhi ya wanataaluma au washirika wetu, jambo linaloharibu taswira ya taaluma
3. Bila kujisahihisha, na kuambiana ukweli, taaluma inaporwa na wasiohusika na itapotea kabisa
4. Kila mwanataaluma kuhakikisha anatenda majukumu yake kwa kufuata sheria taratibu na miongozo iliyowekwa ili kuongeza ufanisi na kuonesha tija na umuhimu wa mfamasia katika sekta ya afya.

TUJITOKEZE KUHESABIWA TAREHE 23/08/2022

SENSA KWA MAENDELEO YA TAIFA

ASANTENI

Benson Katundu.

Katibu Mkuu,

Chama cha Wafamasia Tanzania(PST)

EXECUTIVE

President

Fadhili Hezekiah.

Vice President

Mtani Njeger.

Honorary Secretary

Benson Katundu.

Deputy Secretary

Modekai William.

Treasurer

Jannette Senkondo.